**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO**

# ELIMU SACCOS LTD

# SERA YA MIKOPO

**NAMBA YA USAJILI MGR No. 668**

**YALIYOMO**

**SEHEMU YA KWANZA** ........................................................... 1
1.0 Utangulizi ....................................................................... 1
1.1Madhumuni ya Sera ya Mikopo ............................................. 1
1.2 Walengwa wa sera hii ......................................................... 1

**SEHEMU YA PILI**................................................................... 2
2.0 Utoaji wa mikopo................................................................. 2
2.1Utoaji wa mikopo kwa wanachama ........................................ 2
2.2Sifa za mwanachama anayestahili kupata mkopo ..................... 2
2.3 Maombi ya mkopo .............................................................. 4
2.4 Sababu za kukataliwa kupewa mkopo ................................... 4

**SEHEMU YA TATU** ................................................................. 4
Gharama za Mkopo .................................................................. 4
3.1 Riba, Ada na Adhabu za mikopo .......................................... 4

**SEHEMU YA NNE**.................................................................... 5
4.0 Kinga dhidi ya majanga ya mkopo ........................................ 5
4.1Gharama za kinga ya majanga ya Mkopo ............................... 5
4.2Kazi za mfuko wamajanga ..................................................... 5
4.3Taratibu za kuhudumia mfuko wa majanga ............................. 6

**SEHEMU YA TANO**.................................................................. 6
5.0 Muda wa ukomo wa marejesho ya mkopo ................................ 6
5.1 Ukomo wa kurejesha mkopo ................................................. 6

**SEHEMU SITA** ....................................................................... 6
6. 0 Vyanzo vya kukopesha na Ukomo wa Ukopeshaji ..................... 6
6.1 Vyanzo vya Fedha za kukopesha; .......................................... 6
6.2Ukomo wa ukopeshaji kwa kila aina ya mkopo ......................... 7

**SEHEMU YA SABA** ................................................................... 7
7.0 Uidhinishwaji na Urejeshaji wa Mikopo ..................................... 7
7.1 Uidhinishaji wa maombi ya mikopo ......................................... 7
7.2 Viwango vya mikopo na uidhinishaji........................................ 8

7.3Uidhinishaji wa Bodi ya Chama ............................................. 8
7.4Mikopo kwa viongozi ......................................................... 8
7.5Mikopo kwa watendaji wa chama ......................................... 8
7.6Urejeshaji wa mikopo ......................................................... 9
7.7 Marejesho ya mikopo ........................................................ 9

**SEHEMU YA NANE** ................................................................. 9
8.0 Ukokotoaji na uainishaji wa mikopo iliyocheleweshwa ................ 9
8.1 Adhabu/ tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa mkopo............. 9
8.2Madhara ya ucheleweshaji marejesho ya mkopo..........................10
8.3 Taarifamuhimuzinazopaswakuainishwa kwa mikopo iliyocheleweshwa........................................................................... 10

**SEHEMU YA TISA** ...................................................................10
9.0 Usitishaji wa mapato tarajiwa na marekebisho ya mkopo ..........10
9.1Usitishwaji wa mapato tarajiwa kutoka mikopo cheleweshwa ...11
9.2Mapitio ya kufanya marekebisho ya mikopo ............................11

**SEHEMU YA KUMI** ..................................................................11
10.0Madeni, Matengo na Usimamishaji wa Mikopo kwa Muda ..........11
10.1 Madeni Mabaya...................................................................11
10.2 Matengo ya madeni mabaya ..............................................11
10.3 Kusimamisha mikopo kwa muda .........................................12

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA** ....................................................12
11.0 Ukusanyaji wa Madeni ...........................................................12
11.1Mambo ya kuzingatia kabla ya kukusanya madeni .................12
11.2 Mkataba wa mkusanya madeni ...........................................13

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI** ...................................................13
12.0 Ufutaji wa Mikopo na Uuzaji wa Dhamana ............................13
12.1 Hatua za ufutaji wa mikopo..................................................13
12.2 Taratibu za chama kuuza dhamana za mwanachama ............14

13.0**HITIMISHO** ...........................................................................14

## TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

**ELIMU SACCOS:** Ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo

**MKOPO:** Ni pesa ya mkupuoapewayemwanachamana chama kwa masharti ya kurejesha na riba yake kwa mudamaalum.

**RIBA:** Ni faida itokanayo namkopo kwa mudamaalum.

**DENI:** Ni pesa ambayo mwanachamaanadaiwana chama baada ya kupewamkopo.

**MAREJESHO**: Ni mafungu ya pesayanayotakiwakuletwanamwanachamailikukidhikiwango cha mkopo na riba yake.

**ADHABU:** Ni tozolitokanalona ucheleweshaji wa mkopo kwa mujibu wa mkataba.

**DHAMANA**: Ni maliyoyoteinayowekwa kwa ajili ya kukombolea deni.

**MDHAMINI:** Ni mtu /mwanachamayeyotealiyejitoleakubebamzigowadeniendapomdaiwaatashindwakulipa.

**MUDA:** Ni mafungu ya wakatiyaliyopangwa katika wiki, miezi namiaka.

**MKATABA:** Ni makubaliano baina ya pandembilikwakuzingatiaushahidi wa pandezote.

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

Sera ya Utoaji, ukusanyaji na ufutaji wa mikopo ya Elimu SACCOS ni mwongozo uliowekwa na chama kwa ajili ya kusimamia namna ya utoaji wa mikopo ndani ya chama na ni ramani ya chama inayoonesha namna ya kutoa mikopo kwa wanachama wake. Taratibu hizi za mikopo zimetungwa kwa kuzingatia misingi ya kanuni za utendaji bora wa chama na lazima zifuatwe na zitumike katika shughuli zote za utoaji mikopo kwa wanachama.

Sera hii itazingatia matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni za SACCOS za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2019. Sera hii imejumuisha Maeneo yote muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika usimamizi wa mikopo ikiwa ni pamoja na utoaji wa mikopo, Ukusanyaji wa Mikopo, Ufutaji wa Mikopo, Dhamana za mkopo, taratibu za kuuza dhamana na kinga ya majanga ya mikopo, kama zinavyoelekezwa katika Kanuni ya 28-43 ya Kanuni za SACCOS za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

Sera hii imeandaliwa kwa kuzingatia Sharti Na. 63 la Masharti ya Chama, pamoja na mambo mengine sera itapitiwa mara kwa mara ili kuona kama kunahitaji la kufanya maboresho na bodi itakuwa na jukumu la kuwasilisha maoni na mapendekezo watakayoona yanafaa kwa lengo kuridhiwa na mkutano mkuu kabla ya kufanya maboresho.

### 1.1 Madhumuni ya Sera ya Mikopo

(a) Kuweka misingi na kanuni bora za utoaji mikopo.

(b) Kuepusha migongano isiyo ya lazima katika kutoa mikopo.

(c) Kupunguza hatari ya mikopo mibaya.

(d) Kujenga imani kwa taasisi za ndani na nje, wanachama na wananchi kwa ujumla.

(e) Kuiwezesha Bodi katika usimamizi wa mikopo.

(f) Kutekeleza kwa vitendo Sheria ya Huduma ndogo za fedha Na.10 ya mwaka 2018 na Kanuni za SACCOS za Huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.

### 1.2 Walengwa wa sera hii

**Wadau wa ndani**

(i) Wanachama ndio walengwa wakuu wa Sera hii kwa kuwa ndio wakopaji.

(ii) Watendaji/Wafanyakazi – Hawa ni wataalamu wa kuchanganua na kutathimini mikopo inayoombwa na inayotolewa.

(iii) Wajumbe wa Bodi, Kamati ya Usimamizi – watahusika katika kusimamia na kuhakikisha kuwa taratibu zote za Sera zinafuatwa.

**Wadau wa nje**

i) Wakaguzi wa nje – Watatumia Sera hii wakati wa ukaguzi.

ii) Maafisa Ushirika – Ni washauri katika utekelezaji wa sera hii kama wawakilishi wa Serikali.

iii) Taasisi za Kifedha na wakopeshaji wengine – Watatumia sera hii wakati wa kutoa huduma ya mikopo chamani.

iv) Mrajis wa Vyama vya Ushirika – anahusika na kuidhinisha sera hii na kusimamia utekelezaji wake.

v) Makampuni ya kuchakata taarifa za wakopaji

vi) Waajiri

vii) Benki Kuu ya Tanzania

viii) Wadau wengine

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UTOAJI WA MIKOPO

### 2.1 Utoaji wa mikopo kwa wanachama

Elimu SACCOS itatoa mikopo kwa wanachama wote wenye sifa ya kupata mikopo kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukopesha na kwa kuzingatia sera ya mikopo ya chama bila kuathiri sheria ya Huduma ndogo za fedha na Kanuni za huduma ndogo za fedha zinazosimamia SACCOS za mwaka 2019.

### 2.2 Sifa za mwanachama anayestahili kupata mkopo

Ili kuweka mazingira mazuri ya kuhakikisha mikopo inatolewa, baadhi ya mambo yafuatayo yatazingatiwa kabla mwanachama hajapatiwa mkopo ambapo mwanachama lazima awe na sifa zifuatazo;

(a) Awe mwanachama hai wa Elimu SACCOS alietimiza hisa za msingi na anaechangia akiba kila mwezi kama inavyoelekezwa kwenye Masharti ya Chama.

(b) Awe ametimiza miezi mitatu chamani tangu kujiunga kabla ya kuomba huduma ya mkopo chamani. ( Hii itategemea na uwezo wa chama kumhudumia mwanchama husika)

(c) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa wakati wa kuomba mkopo mwingine.

(d) Asiwe na mkopo alioshindwa kulipa kutoka taasisi nyingine.

(e) Awe na historia nzuri chamani katika urejeshaji wa mikopo yake

(f) Awe mshiriki mzuri kwenye shughuli za chama

(g) Awe na mradi unaotengeneza faida

(h) Awe na wadhamini wawili wenye akiba na hisa toshelezi kudhamini mkopo anaoomba.

**Pamoja na sifa zilizoainishwa katika sehemu hii pia mambo yafuatayo yatazingatiwa kama sifa ya mwanchama kuweza kupatiwa mkopo.**

**A. TABIA (CHARACTER)**

Tabia ya mkopaji itatathiminiwa kikamilifu kulingana na kumbukumbu zake za ukopaji na urejeshaji wa mikopo yake. Wanachama, Kamati ya Usimamizi, Kamati ya mikopo au kiongozi yeyote wa chama anayeweza kuwa sehemu ya kujua tabia ya mkopaji na anaweza kutoa maoni juu ya mkopaji husika.

Dhamana kubwa iliyopita kiwango cha mkopo haitakuwa kigezo cha kumpa mkopo mwanachama aliye na tabia au historia mbaya katika ukopaji na urejeshaji wa mikopo.

Wakopaji wapya watatathiminiwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kufanya marejesho na kuchambua mikopo yao kupitia taasisi za uchakataji wa taarifa za wakopaji (Credit reference bureau).

**B. HALI (CONDITION)**

Hali ya utoaji wa mkopo kwa mwanachama itazingatia mambo ya nje yanayoathiri mkopo wa mwombaji ikiwa ni pamoja na

i. Hali ya uchumi wa nchi

ii. Thamani ya pesa

iii. Sheria za nchi

iv. Hali ya soko la biashara inayoombewa mkopo

v. Hali ya soko la kazi/ajira

vi. Na mambo mengine yanayoathiri hali ya urejeshaji mkopo.

**C. UWEZO WA MTIRIRIKO WA KIFEDHA**

Uwezo wa kurejesha mkopo ndio kitu cha kwanza na cha msingi cha kuangalia katika kutathimini uwezo wa mwanachama kurejesha mkopo anaoomba kwa kutegemea shughuli za kiuchumi

**D. DHAMANA YA MKOPO (COLLATERAL)**

Dhamana itakayowekwa/zitakazowekwa na mwanachama wakati wa kuomba mkopo zitatakiwa kuwa na thamani zaidi ya kiwango cha mkopo utakaoombwa. Aidha, tathimini halisi ya thamani ya dhamana itakayowekwa na wanachama itatakiwa kutathiminiwa vizuri kabla ya kuwekwa kwenye dhamana ya mkopo. *(Mthaminishaji anayetambuliwa na serikali).*

**2.3 Maombi ya mkopo**

Mwanachama kabla ya kupatiwa mkopo atapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

(a) Atachukua fomu chamani ataijaza na kuirudisha kwa utaratibu ulioelekezwa katika fomu hiyo.

(b) Mwanachama atalipia gharama za fomu ya maombi ya mkopo kwa kiasi kilichopangwa na mkutano mkuu.

(c) Mwanachama atalipia 1% ya mkopo kwa ajili ya kushughulikia mkopo huo.

(d) Mwanachama ataomba kiasi cha Mkopo kulingana na hitaji lake.

(e) Mwanachama atalazimika kuambatisha vielelezo vyote muhimu kama fomu inavyoelekeza.

(f) Atakuwa tayari kutoa ridhaa kwa chama kutoa taarifa zake za mikopo kwa mamlaka za uchakati wa taarifa za wakopaji nchini pasipo hata kutaarifiwa.

**2.4 Sababu za kukataliwa kupewa mkopo**

Kwa kuzingatia kanuni ya 32 ya Kanuni za SACCOS za huduma ndogo za fedha zinazosimamia SACCOS, kamati ya mikopo itapaswa kumtaarifu

mwanachama kwa maandishi ikiwa itaona mwanachama husika hajakidhi vigezo vya kupata mkopo ndani ya siku saba baada ya kufanya maamuzi ya kumnyima mkopo huo.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 GHARAMA ZA MKOPO

### 3.1 Riba, Ada na Adhabu za mikopo

Kiwango cha riba, ada, adhabu na gharama nyingine za mikopo vitapendekezwa na Bodi ya Chama na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa wanachama. Aidha, kiwango cha riba kitawekwa baada ya kufanyika uchambuzi maalum utakaonyesha kiwango cha riba kilichowekwa kitanufaisha wanachama na kuweza kumudu gharama za uendeshaji wa shughuli za chama na mahitaji mengine ya chama kwa kuzingatia ulazima uliopo.

Viwango vya riba, ada, adhabu na gharama nyingine vitafanyiwa marejeo ya mara kwa mara ili kuona kama vinaendana na wakati na vinaweza kubadilishwa baada ya kuridhiwa na Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis.

Mikopo yote italipiwa riba kwa kila mwezi kama inavyofafanuliwa kwenye Sera hii kwa kuzingatia jedwali Na.1

**Jedwali Na.1 Viwango vya Ada, Riba na Adhabu**

| Aina ya Mkopo | Ada ya Mkopo | Riba (%) | Adhabu (%) x Rejesho lilocheleweshwa |
|---|---|---|---|
| Uzalishaji | **1%** | **1%** | |
| Dharura | **0%** | **7%** | |

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 KINGA DHIDI YA MAJANGA YA MKOPO

### 4.1 Gharama za kinga ya majanga ya Mkopo

Elimu SACCOS itakuwa na mfumo maalum wa majanga kwa kila mkopo unaochukuliwa isipokuwa mkopo wa **dharura** na kiasi hicho kitahifadhiwa katika akaunti maalum kwa lengo la kulinda mikopo ambayo haitarejeshwa. Viwango vya (kuchangia) itakuwa kama ifuatavyo;

| Muda wa mkopo (miezi) | % ya mkopo |
|---|---|
| **0 – 12** | **0.99** |
| **13 – 36** | **1.54** |
| **37 – 60** | **2.09** |

### 4.2 Kazi za mfuko wa majanga;

i. Kufidia deni la mkopo wenye majanga kwa mwanachama aliyefariki baada ya dhamana kutokidhi.
ii. Kufidia deni la mkopo wenye janga wa mwanachama mwenye ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari mwenye taalum husika.
iii. Kutoa rambirambi kama itakavyopangwa na mkutano mkuu kwa mrithi halali wa marehemu aliyekuwa na mkopo wenye kinga.
iv. Robo ya fedha ya mfuko wa majanga itatumika kwenye miradi ya chama iwapo mfuko huo utazidi nusu ya jumla ya hisa na akiba zote za wanachama kwa idhini ya mkutano mkuu wa chama.

(a) Uhifadhi wa fedha ya mfuko wa majanga ya mkopo. Fedha hii itatunzwa kwenye akaunti maalumu itakayoitwa akaunti ya majanga.

(b) Atakayetoa fedha katika akaunti ya majanga, kinyume na kazi tajwa hapo juu (b) i-iv) atakabiliwa na mambo yafuatayo:-
   i. Ataondolewa/ kufukuzwa uanachama
   ii. Atafilisiwa
   iii. Atachukuliwa hatua za kisheria.

(c) Watia saini watakuwa ni;
   i. Wajumbe wa Bodi ya Chama
   ii. Mwenyekiti Kamati ya Usimamizi
   iii. Watia saini katika akaunti hii ya majanga watadumu wa miaka 3

### 4.3 Taratibu za kuhudumia mfuko wa majanga

a. Fedha za mfuko wa majanga ya mkopo zitawasilishwa benki katika akaunti maalum mara baada ya mwanachama kupatiwa mkopo

b. Fedha za mfuko zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia mahitaji yatayojitokeza.

c. Ikiwa mfuko haujaimarika vya kutosha kuweza kumudu mahitaji yanayojitokeza kiasi kinachodaiwa kinaweza kusubiri mfuko uimarike ndipo kilipwe.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MUDA WA UKOMO WA MAREJESHO YA MKOPO

### 5.1 Ukomo wa kurejesha mkopo

Mwanachama atarejesha mkopo wake kwa utaratibu aliopangiwa na kwa namna yeyote ile muda wa juu wa kurejesha mkopo hautazidi miaka mitano.

**Jedwali Na. 2 Aina ya mikopo na muda wa marejesho**

| Aina ya Mkopo | Muda wa marejesho |
|---|---|
| Uzalishaji | Mwezi 1 hadi miezi 60 |
| Dharura | Mwezi 1-3 |
| | |
| | |

Riba ya mkopo wa uzalishaji itatokana na kanuni ifuatayo.

$$\text{Faida} = \text{mkopo}\ \frac{(1+t)i}{200}$$

Ambapo; (**t**) ni*muda* katika miezi, (**i**) ni *kiwango cha riba* ambacho ni **1**%

Mkopo wa dharura riba ni **7%** au itakavyoamriwa vinginevyo na Mkutano Mkuu.

**SEHEMU SITA**

## 6. 0 VYANZO VYA UKOPESHAJI NA UKOMO WA MIKOPO

### 6.1 Vyanzo vya Fedha za kukopesha

Fedha za kutoa mikopo chamani zinaweza kutoka katika maeneo yafuatayo**;**

(a) Hisa za wanachama

(b) Malimbikizo ya faida

(c) Mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha na zisizo za kifedha.

(d) Misaada kutoka kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi.(kwa kuzingatia masharti)

### 6.2 Ukomo wa ukopeshaji kwa kila aina ya mkopo

Katika Elimu SACCOS kiwango cha juu katika kila mkopo bila kuathiri matakwa ya kanuni ya 33(1) ya Kanuni za SACCOS za huduma ndogo za fedha itakuwa kama ifuatavyo.

a) Uzalishaji 25,000,000/=

b) Dharua 300,000/=

**NB:** Kiwango chochote cha juu cha mkopo kinaweza kupangwa/ kufanyiwa marekebisho wakati wowote na mkutano mkuu.

**SEHEMU YA SABA**

## 7.0 UIDHINISHWAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO

### 7.1 Uidhinishaji wa maombi ya mikopo

(a) SACCOS haitatoa mkopo bila idhini ya Kamati ya Mkopo

(b) Kamati ya Mikopo haitaidhinisha mkopo kama sehemu ya mkopo haijadhaminiwa au mkopo haujazaminiwa kikamilifu

(c) Kamati ya mkopo itaridhia ombi la mkopaji kupewa mkopo baada ya kujiridhisha na uwezo wa mwanachama kufanya marejesho

(d) Kamati ya mikopo ina haki ya kukataa/kukubali au kurudisha ombi la mkopo kwa mwanachama ikiwa mwanachama atakuwa hakutimiza vigezo vya kupewa mkopo kama ilivyoelekezwa katika sehemu ya 2.1 ya sera hii.

(e) Ikiwa ombi la mkopo halijakubaliwa SACCOS itamfahamisha mwanachama sababu za kukatatiliwa kwa ombi lake ndani ya kipindi cha siku saba.

(f) Fedha za mikopo zitatolewa kutegemeana na hali ya ukwasi chamani lakini kwa namna yeyote ile mikopo midogo itapewa kipaumbele na ikiwa hali ya ukwasi wa chama iko chini.

(g) Kamati ya mikopo haitaidhinisha kiwango cha mikopo kinachozidi shilingi **15,000,000/=**

(h) Kamati ya kitaalamu haitaidhinisha kiasi cha mikopo kinachozidi shillingi **15,000,000/=**

(i) Kiasi cha mkopo kinachozidi shilingi **15,000,000/=** kitaamuliwa na Bodi ya Chama

(j) Meneja wa chama ataruhusiwa kuidhinisha mikopo yote ya dharura kwa wanchama wenye sifa za kukopa mara baada ya Afisa Mikopo kujiridhisha uwezo wa mkopaji katika kurejesha mkopo husika wa dharura

(k) Kamati ya mikopo/kamati ya kitaalamu itatumia kumbukumbu zifuatazo ili kufikia uamuzi wake;

i) Mali anazotumia mwanachama kudhamini mkopo

ii) Daftari linaloonyesha orodha ya wanachama

iii) Uzoefu katika shughuli anayoombea mkopo

iv) Aina ya mradi unaoombewa mkopo

v) Mahali mradi ulipo

vi) Pamoja na vigezo vingine vitakavyowekwa na chama.

vii) Kanuni ya 30 ya Kanuni za SACCOS za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019

### 7.2 Viwango vya mikopo na uidhinishaji

**a) Uidhinishaji wa kamati ya mikopo**

Uidhinishaji wa mikopo utakua chini ya kamati ya mikopo au kamati ya kitaalam na kamati ya mikopo au kamati ya kitaalam haitaidhinisha mkopo unaozidi kiasi cha shilingi **15,000,000/=** kiasi kitakachozidi **15,000,000/=** kitaamuliwa na Bodi ya chama.3.

**b) Uidhinishaji wa meneja**

Katika Elimu SACCOS meneja atakuwa na mamlaka ya kuidhinisha mikopo yote ya dharura isiyozidi kiasi cha shilingi **300,000/=** baada ya Afisa Mikopo kujiridhisha kama mkopaji anaweza kufanya marejesho kwa mkopo huo, mikopo mingine itafuata taratibu zilizoainishwa katika sera hii.

### 7.3 Uidhinishaji wa Bodi ya Chama

Bodi itakuwa na jukumu la kuidhinisha mikopo yote inayozidi kiasi cha shilingi **15,000,000/=** ambayo kamati ya mikopo, kamati ya kitalaam na menejimenti hawawezi kuidhinisha kama ilivyoelekezwa katika sera hii.

### 7.4 Mikopo kwa viongozi

i. SACCOS haitatoa mkopo kwa mjumbe wa Bodi au mjumbe wa kamati yeyote kabla ya kupata idhini kutoka kwa wajumbe wa Bodi.

ii. Mjumbe wa Bodi au wa kamati hatoruhusiwa kuwa miongoni wa wajumbe wa kikao wakati wa kupitisha mkopo wake.

### 7.4 Mikopo kwa watendaji wa chama

i. SACCOS itatoa mikopo kwa watendaji ambao ni wanachama.

ii. SACCOS haitatoa mkopo kwa mtendaji au mtu mwenye mahusiano ya karibu na chama kwa namna yeyote ile kabla ya kupata idhini kutoka kwa kamati ya mikopo.

iii. Mikopo ya wajumbe wa Bodi na watendaji wakuu itajadiliwa na Bodi ya chama.

**Kwa namna yeyote ile SACCOS haitatoa mkopo kwa upendeleo, kwa viwango tofauti vya riba tofauti na vile anavyotozwa mwanachama mwingine.**

### 7.5 Urejeshaji wa mikopo

(a) Mwanachama atafanya marejesho ya mkopo pamoja na riba kwa kupitia akaunti ya chama na kama itakavyopangwa na Mkutano Mkuu.

(b) Ikiwa mwanachama atalipa kiasi cha mkopo wake au kulipa mkopo wote kwa mkupuo hatapaswa kulipa riba ya muda ambao hakukaa na mkopo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 37(2) ya kanuni za SACCOS za mwaka 2019.

### 7.6 Marejesho ya mikopo

(a) Kila mwanachama ana wajibu wa kuhakikisha anafanya marejesho yake kwa mikopo aliyochukua chamani kwa njia zifuatazo;

i. Makato hazina toka kwenye mshahara wake

ii. Kuweka moja kwa moja kwenye akaunti ya chama (mkononi)

iii. Zote mbili kwa pamoja yaani (i )na (ii)

(b) Kamati ya Mikopo/Meneja watahusika mara kwa mara kutengeneza taarifa ya hali halisi ya mikopo ya wanachama kila mwezi ili kutoa hali halisi ya mikopo inayohitaji kufatiliwa kwa karibu zaidi.

(c) Taarifa zitaonyesha hali halisi ya maendeleo ya mikopo na zitawasilishwa mbele ya Bodi kila baada ya robo mwaka na kuwekwa kwenye mbao za matangazo na sehemu ambazo wanachama wanapatikana.

(d) Wadhamaini wa mkopo watatakiwa kuhakikisha mkopaji anarejesha marejesho yake kwa mujibu wa jedwali la marejesho yake.

## SEHEMU YA NANE

### 8.0 UKOKOTOAJI NA UAINISHAJI WA MIKOPO ILIYOCHELEWESHWA CHAMANI.

Chama kitaandaa taarifa za ukokotoaji wa mikopo iliyocheleweshwa kwa kuanzia tarehe ya mwisho ambayo rejesho la mkopo husika lilifanyika mpaka pale malipo yote yatakapokuwa yamekamilika.

### 8.1 Adhabu/tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa mkopo.

| Idadi ya siku za kuchelewesha | Tozo / faini |
|---|---|
| **0-2** | 0% |
| **3-30** | 1% |
| **31-180** | 30% |
| **181-365** | 50% |
| **365+** | 100% |

**NB**: Gharama ya ufuatiliaji itapangwa na mkutano mkuu itakayoambatana na tozo kwa kiasi kisichorejeshwa kulingana na asilimia kwa kila muda kama ilivyoainishwa hapo juu.

Mikopo iliyocheleweshwa itakokotolewa kila mwezi na kutolewa taarifa siku ya mwisho wa mwezi ambapo mikopo hiyo itaainishishwa katika makundi yafuatayo:-

**Jedwali Na.3 Makundi na Hali ya Ucheleweshaji.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji |
|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 |

### 8.2 Madhara ya ucheleweshaji marejesho ya mkopo

Mwanachama aliyecheleweshа marejesho ya mkopo atapata madhara yafuatayo:-

(i) Kufungiwa akiba zake
(ii) Kufungwa kwa akiba za wadhamini wake
(iii) Kutozwa faini kwa kuzingatia kipengele (8.1)
(iv) Kuingizwa katika makundi ya warejeshaji wabaya kama ifuatavyo
- (a) Kundi angalizo (siku 31 – 90)
- (b) Kundi la chini ya kiwango (siku 91 – 180)
- (c) Kundi mashaka (siku 181-365)
- (d) Kundi chechefu (+365)

(v) Akiba za wadhamini zitakatwa kufidia deni la mkopaji
(vi) Mwanachama aliyewahi kuingizwa katika kundi mashaka na chechefu zaidi ya mara moja, punde amalizapo mkopo, ataelimishwa na hataruhusiwa kuchukua mkopo mwingine kwa siku 30

### 8.3 Taarifa muhimu zinazopaswa kuainishwa kwa mikopo iliyocheleweshwa

Taarifa ya ucheleweshwaji wa mikopo itajumuisha mambo yafuatayo;

i. Jina la mwanachama, anuani na mawasiliano yake binafsi
ii. Tarehe mkopo ulipotolewa
iii. Mkopo halisi uliotolewa na bakaa la deni linalodaiwa ambalo halijarejeshwa chamani
iv. Majina ya wadhamini na dhamana ya mkopo iliyowekwa.

## SEHEMU YA TISA

## 9.0 USITISHAJI WA MAPATO TARAJIWA NA MAREKEBISHO YA MKOPO

### 9.1 Kusitishwaji mapato tarajiwa kutokana na mikopo iliyocheleweshwa

Chama na mikopo kutoka kitasitisha riba zote tarajiwa ambazo zitakuwa zimekadiriwa kupatikana kwenye mwaka husika kutokana na mikopo iliyocheleweshwa iwapo mkopo uliotolewa hautalipwa kwa siku tisini. Aidha, chama kitaondoa mapato tarajiwa yanayotokana katika akaunti ya mapato tarajiwa.

### 9.2 Mapitio ya kufanya marekebisho ya mikopo

Elimu SACCOS haitafanya marekebisho ya mkopo zaidi ya mara moja kwa wanachama wake watakaopewa mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati.

i. Mkopo wowote ambao umefanyiwa marekebisho au mabadiliko katika masharti yake ya awali, hautapaswa kuainishwa kama "upo katika daraja zuri" isipokuwa marejesho ya mkopo huo yamefanyika kikamilifu angalau mara nne mfululizo tangu mkopo ulipofanyiwa marekebisho.

ii. Iwapo mkopo utafanyiwa marejesho kikamilifu mara nne mfululizo, mkopo huo utaainishwa kama mkopo usiocheleweshwa.

iii. Elimu SACCOS itatoa taarifa ya mikopo yote iliyofanyiwa marekebisho kama taarifa inayojitegemea katika mizania ya hesabu ya chama 42(2).

## SEHEMU YA KUMI

## 10.0 MADENI, MATENGO NA USIMAMISHAJI WA MIKOPO KWA MUDA

### 10. 1 Madeni Mabaya

(a) Madeni mabaya ni yale yatakayokuwa yameshindwa kurejeshwa katika kipindi kinachozidi siku 30 kama ilivyofafanuliwa katika kanuni ya 40 (1)(2) ya kanuni za huduma ndogo za fedha (SACCOS) za mwaka 2019

(b) Madeni mabaya yatafutwa katika mahesabu ya chama yatakapokuwa yamefikia zaidi ya miezi kumi na mbili (12) kwa kuzingatia Kanuni ya 43 ya kanuni za SACCOS za mwaka 2019.

(c) Chama kitaendelea kufuatilia madeni hayo na yakilipwa yataingizwa kama mapato mengineyo kwa kuzingatia taratibu za kihasibu.

### 10.2 Matengoya madeni mabaya

Chama kitafanya matengo ya mikopo mibaya kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019.
Elimu SACCOS itatenga 15% kutoka katika faida yake ya mwaka kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa na wanachama kwa kuzingatia kanuni Na. 40(3) ya kanuni za huduma ndogo za Fedha (SACCOS) za mwaka 2019 ili kufidia kiasi cha mikopo hiyo mibaya kama inavyoainishwa katika jedwali Na.2

**Jedwali Na.2 Matengo ya Mikopo Mibaya.**

| Na. | Makundi ya Uchelewaji | Hali ya Uchelewaji | Kiasi cha matengo (% ya bakaa kwa mkopo uliochelewa) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mikopo iliyopo kwenye angalizo | Siku 31-90 | 10% |
| 2. | Mikopo iliyo chini ya Kiwango | Siku 91-180 | 30% |
| 3. | Mikopo yenye mashaka | Siku 181-365 | 50% |
| 4. | Mikopo mibaya/Hasara | Zaidi ya siku 365 | 100% |

**Kiasi cha tengo litakalotengwa kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa kitawekwa kwenye akaunti maalum ya mikopo mibaya.**

### 10.3 Kusimamishamikopo kwa muda

(a) Chama kinaweza kusimamisha utoaji wa mikopo kulingana na mwenendo wa ulipaji wa mikopo hiyo.

(b) Ikiwa ni Mikopo mingi ambayo ipo mikononi mwa wanachama na haijakusanywa na hivyo kuhatarisha hali ya ukwasi katika chama "liquidity crisis".

(c) Endapo Mrajis wa Vyama vya Ushirika atafanya ukaguzi na kubaini na kujiridhisha kuwa hali halisi ya kifedha ni mbaya.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

### 11. O UKUSANYAJI WA MADENI

Mikopo yote itakayotolewa na chama kwa wanachama wake itapaswa kulipwa chamani kwa utaratibu uliopangwa na ikiwa utaratibu uliowekwa hautafatwa na wakopaji chama kitakuwa na jukumu la kufuatilia na kuhakikisha madeni yote yanakusanywa.

### 11.1 Mambo ya kuzingatia kabla ya ukusanyaji wamadeni

Chama kitaendelea kuhakikisha madeni yote yanakusanywa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kati ya mkopaji na mkopeshaji na mambo yafuatao yakibainika ufatiliaji wa karibu utahitajika, aidha miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na;

i. Malipo ya marejesho ya mwanachama yatakuwa pungufu ya malipo yaliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba uliosainiwa na mwanachama kipindi anachukua mkopo.
ii. Endapo malipo ya marejesho ya mwanachama hayatafanyika ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) tangu marejesho hayo kutakiwa kufanyika bila kujali kuwa mkopo uliocheleweshwa ni riba au riba na mkopo msingi.
iii. Iwapo jedwali la marejesho ya mkopo lililopo kwenye fomu ya mikopo halitazingatiwa katika marejesho ya mkopo ya mwanachama.

### 11.2 Mkataba wa mkusanya madeni

Chama kinaweza kuingia mkataba na mkusanya madeni endapo itaonekana mkopaji amechelewesha marejesho na jitihada za chama kufanya ufuatiliaji zimeshindwa kuzaa matunda na hatimaye kuona umuhimu wa kuweka mkusanya madeni.

Bila kuathiri maelekezo mengine hapo juu, mkusanyaji wa madeni atapaswa kupata ada yake moja kwa moja kutoka kwa mdaiwa
Aidha chama kinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuingia mkataba na mkusanya madeni;

i. Kuhakikisha mkusanya madeni ana kibali maalum cha kufanya kazi hiyo kutoka mamlaka halali za serikali (TCDC)

ii. Kujiridhisha mahali na sehemu mtoa huduma anafanyia kazi zake

iii. Kuangalia historia ya mtoa huduma.

iv. Kuhakikisha mtoa huduma analinda haki za mwanachama wakati wa kukusanya madeni

v. Kuhakikisha mkusanya madeni anakusanya deni kwa kuzingatia mkataba na makubaliano yaliyopo kwenye fomu ya mkopo na mkataba wa mkopo

vi. Kuhakikisha mkusanya madeni anatambua vema mali za mkopaji zilizotumika kudhamini mkopo

vii. Kufanya tathmini na kujiridhisha kama mkusanya madeni ana uwezo na vifaa vitakavyomsaidia kufanya kazi hiyo pasipo kukigharimu chama.

viii. Mkataba uainishe haki na wajibu za pande zote na upite kwa mwanasheria kwa ajili ya kulinda haki za pande zote

ix. Mkataba wa mkusanya madeni na chama utapitishwa kwa Mrajis ili aone kama mkataba husika haujaegemea upande mmoja

x. Kuhakikisha taratibu zote zitakazochukuliwa na Mkusanya madeni, zinalinda haki ya mwanachama na chama kwa ujumla.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## 12.0UFUTAJI WA MIKOPO NA UUZAJI WA DHAMANA

### 12.1 Hatua za ufutaji wa mikopo

Elimu SACCOS itafuta mikopo yake kutoka katika mizania yake endapo:

(a) Mkopo utacheleshwa kurejeshwa kwa zaidi ya siku 365;
(b) Chama kitapoteza haki zake za kimkataba zinazohusiana na mkopo husika;
(c) Chama kimekosa haki kisheria katika dai la mkopo husika
(d) Mkopo utakapoonekana hauwezi kukusanywa;
(e) Hakuna uwezekano wa chama kukusanya mkopo kutokana na hukumu ya mahakama.
(f) Dhamana zote zilizodhamini mkopo, zimetathiminiwa na kuuzwa, na mapato yanayotokana na mauzo yameshindwa kufuta mkopo unachodaiwa
(g) Chama hakina uwezo wa kukusanya mkopo au hakuna dhamana au jitihada za kukusanya deni zimeshindikana.
(h) Ikiwa chama kina tengo la mikopo mibaya linalotosha kufuta mkopo.

**Iwapo mkopo wa mwanachama utafutwa kwenye vitabu vya chama na kama mwanachama huyo atakuwa hajatangazwa kufilisika, mkopo huo utapaswa kufuatiliwa na kukusanywa kama mikopo mingine.**

### 12.2 Taratibu za chama kuuza dhamana za mwanachama

Ili kufidia mikopo mibaya chama kinaweza kuuza dhamana za mwanachama. Aidha Kabla chama hakijauza dhamana za mwanachama kitapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

i. Akiba na hisa za hiyari za mwanachama zimechukuliwa katika akaunti ya mwanchama lakini hazijatosheleza kulipa deni husika la mwanchama
ii. Wadhamini wamepatiwa taarifa na kushindwa kutoa ushirikiano wa kutosha kuhakikisha deni la mkopaji limelipwa.
iii. Ikiwa mwanachama ana dhamana zaidi ya moja dhamana itakayouzwa ni ile tu inayoweza kukidhi deni husika na dhamana

zilizobaki zinaweza kurudishwa baada ya kujiridhisha deni husika limelipwa kikamilifu.

iv. Chama kitalazimika kurudisha kiasi cha fedha kilichobakia mara baada ya dhamana kuuzwa na kufuta mkopo
v. Chama kinaweza kuuza dhamana za mdhamini baada ya akiba, hisa na dhamana za mkopaji mwenyewe kushindwa kulipia mkopo.

## 13.0 HITIMISHO

Sera hii imetayarishwa na Bodi ya Elimu SACCOS na kupitishwa na wanachama katika Mkutano Mkuu uliofanyika tarehe **24** Mwezi **10**, mwaka **2020**. Na itaanza kutumika tarehe **01**, mwezi **01**, mwaka **2020** baada ya kuidhinishwa na **Mrajis**.

______________________________

**Mrajis wa Vyama vya Ushirika**

Tarehe__________________